

Changamoto za DD Kanda ya Iringa



Barabara ya kuelekea Nambendo

Bohari ya Dawa (MSD) ilianza kutumia mfumo wa ugavi shirikishi wa usambazi dawa na vifaa tiba moja kwa moja (Direct Delivery - DD) hadi kwenye vituo vya kutolea huduma za afya mnamo mwaka 2013.

Mfumo huu ulianza kutumika badala ya mfumo wa awali wa kufikisha dawa na vifaa tiba mpaka kwa waganga wakuu wa mikoa na wilaya ambao wao walikuwa na jukumu la kupeleka kwenye vituo vya kutolea huduma za afya.

Mfumo wa usambazi dawa na vifaa tiba moja kwa moja (DD) ulilenga kuondoa changamoto za ucheleweshaji wa usambazaji wa dawa na vifaa tiba.

Katika utekelezaji wake mfumo wa DD unakabiliwa na changamoto mbalimbali hasa kwenye maeneo magumu kufikika.

Iringa ni kati ya kanda moja wapo za MSD zinazo

tekeleza mfumo huu. Kanda hii inasambaza dawa na vifaa tiba katika vituo vya afya na zahanati takribani 505 vilivyopo katika mikoa ya Iringa na Ruvuma .

Kanda imekuwa ikikutana na changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa mfumo huu, zikiwemo za miundo mbinu ambayo mingi hali yake sio nzuri, hasa ile inayokwenda kwenye vituo vya afya na zahanati zilizopo vijijini.

Kipindi cha mvua barabara nyingi zinakuwa na mashimo na matope hivyo inawia vigumu kwa magari yanayosambaza dawa na vifaa tiba kuvifika vituo hivyo katika hali salama

Changamoto kubwa imeshuhudiwa mwanzoni mwa mwezi wa tatu 2016, kipindi cha usambazaji wa dawa na vifaa tiba kwenda katika vituo vya Nambendo, Magwamila na Muhukulu karibu na mpaka wa nchi ya Tanzania na Msumbiji mkoa wa Songea

Katika tukio hilo, gari la MSD (kwenye picha) likiendeshwa na Ndugu Rodgers Kapingo (Dereva wa Kanda ya Iringa) lililokuwa na dawa llinasa katika matope. Dereva alilazimika kuomba msaada kutoka kwa wananchi wa eneo lile ili kulitoa gari katika matope.

Baada ya kulikwamua gari kutoka kwenye matope kwa msaada wa wananchi, dereva alifanikiwa kuzifikisha na kukabidhi dawa kwenye vituo vyote vya afya alivyopangiwa kwa usalama.



Barabara ya kuelekea Nambendo